

Mwongozo wa Marejeleo ya Dozi za Kuongeza Nguvu ya Chanjo ya COVID-19 kwa Watu wa Umri Wote



Wewe au mwanao alichanjwa kwa matoleo ya msingi ya chanjo ya COVID-19 ili kukulinda na kuwalinda wengine dhidi ya kuumwa sana, kulazwa hospitalini, na hata dhidi ya kifo kinachoweza kusababishwa na COVID-19. Uchunguzi unaonyesha kwamba japo kuwacha chanjo za COVID-19 huendelea kuwana ufanisi, lakini uwezo wa kewa kukulinda hapunguaba adaya muda fulani.

Kwa sasa, kukuongezea nguvu imebaki kuwa njia yenye ufanisi zaidi wa kukulinda.

Tazama chati iliyopo hapo chini ili kutambua kamawewe au mwanao anastahiki kupata dozi moja au zaidi za kuongeza nguvu chanjo ya COVID-19.*

	Ni nani anastahiki?	Ni muda gani ninapaswa kupata dozi ya kuongeza nguvu?	Je, ninaweza kupata dozi ya pili ya kuongeza nguvu?	Dozi ipi ya kuongeza nguvu?
<p><i>Ikiwa ulipokea...</i></p> <p>Pfizer</p>	<p>Kila mtu mwenye umri wa miaka 5 na zaidi anapaswa kupata dozi ya kuongeza nguvu ili kwenda na wakati.</p>	<p>Walau miezi 5 baada ya kukamilisha chanjo ya Pfizer ya matoleo ya msingi.</p>	<p>Kila mtu mwenye umri wa miaka 50 na zaidi anapaswa kupata dozi ya pili ya kuongeza nguvu walau miezi 4 baada ya kupata dozi ya kwanza ya kuongeza nguvu.</p>	<p>Watu wazima wenye umri wa miaka 18 na zaidi wanaweza kupata dozi yoyote ya kuongeza nguvu ya chanjo ya mRNA COVID-19.</p> <p>Watoto wenye umri wa 5-17 wanapaswa kupata dozi ya Pfizer ya kuongeza nguvu.</p>
<p><i>Ikiwa ulipokea...</i></p> <p>Moderna</p>	<p>Watu wazima wenye umri wa miaka 18 na zaidi wanapaswa kupata dozi ya kuongeza nguvu ili kwenda na wakati.</p>	<p>Walau miezi 5 baada ya kukamilisha chanjo ya Moderna ya matoleo ya msingi.</p>	<p>Kila mtu mwenye umri wa miaka 50 na zaidi anapaswa kupata dozi ya pili ya kuongeza nguvu walau miezi 4 baada ya kupata dozi ya kwanza ya kuongeza nguvu.</p>	<p>Dozi yoyote ya kuongeza nguvu ya chanjo ya mRNA COVID-19.</p>
<p><i>Ikiwa ulipokea...</i></p> <p>Johnson & Johnson</p>	<p>Watu wazima wenye umri wa miaka 18 na zaidi wanapaswa kupata dozi ya kuongeza nguvu ili kwenda na wakati.</p>	<p>Walau miezi 2 baada ya kukamilisha chanjo ya J&J ya matoleo ya msingi.</p>	<p>Kila mtu mwenye umri wa miaka 50 na zaidi na wale waliopata chanjo ya J&J kama dozi yao ya msingi na ya kuongeza nguvu, wanapaswa kupata dozi ya pili ya kuongeza nguvu walau miezi 4 baada ya kupokea dozi ya kwanza ya kuongeza nguvu.</p>	<p>Kwa dozi ya kwanza ya kuongeza nguvu, dozi ya chanjo ya mRNA ni inapendwazaidi ya J&J. Dozi ya pili ya kuongeza nguvu inapaswa kuwa chanjo yoyote ya mRNA COVID-19.</p>
<p><i>Ikiwa ulipokea...</i></p> <p>Novavax</p>	<p>Ikiwa ulipata Novavax katika misururu yako ya msingi, hustahiki kupokea dozi ya ziada ya chapa yoyote wakati huu.</p>			

Ikiwa kingamaradhi yako imeathiriwa kiasi au vibaya, miongozo itatofautiana.

*Watu ambao walipata maambukizi ya SARS-CoV-2 hivi karibuni wanaweza kuzingatia **kucheleweshwa dozi ya kwanza au pili ya kuongeza nguvu ya chanjo ya COVID-19 kwa miezi 3 kutoka walipoona dalili au walipofanyiwa kipimo (iwapo maambukizi hayakuonyesha dalili)**. **Uchunguzi umeonyesha (Kiingereza pekee)** kucheleweshwa kwa muda kati ya maambukizi na kupata chanjo kunaweza kuimarisha mwitikio wa kinga kwa chanjo. Pia, kumeonekana uwepo wa hatari ndogo ya kupata maambukizi tena ndani ya majuma mpaka miezi kadhaa kutoka yalipotokea maambukizi ya awali. Sababu binafsi kama vile hatari ya **ugonjwa mbaya wa COVID-19** (Kiingereza pekee), **daraja la jamii la COVID-19** (Kiingereza pekee), au tabia za aina ya SARS-CoV-2 inayopatikana zaidi, zinapaswa kuzingatwa wakati wa kufanya maamuzi ya kusogeza mbele muda wa kupata dozi ya kuongeza nguvu baada ya maambukizi.

Maswali ya Mara kwa Mara Kuhusu Dozi za Kuongeza Nguvu za Chanjo ya COVID-19

Kwa nini dozi za kuongeza nguvu ni muhimu?

Dozi za kuongeza nguvu zitakupatia ulinzi endelevu dhidi ya ugonjwa mbaya. Hapo awali, matumizi ya dozi za kuongeza nguvu yalipendekezwa kwa baadhi ya watu ambao walikuwa kwenye hatari kubwa ya kupata maambukizi mabaya ya COVID-19, lakini mapendekezo yameongezwa na kujumuisha kila mtu mwenye miaka 5 na zaidi aliyepokea chanjo ya Pfizer ili kuongeza uwezo wa kujikinga dhidi ya ugonjwa wa COVID-19. Baadhi ya maeneo ya watu, kama vile wale ambao wanaumwa kiasi hadi wale walio na shida kubwa kwenye kinga ya mwili, wanaweza kuhitaji dozi za nyongeza ili kuimarisha kinga. Hii ni muhimu hasa kwa ongezeko la aina zinazosambaa zaidi na visa vya COVID-19 kuongezeka Marekani.

Iwapo kuna uhitaji wa dozi za kuongeza nguvu, je, hii inamaanisha kuwa chanjo hazifanyi kazi?

Hapana. Chanjo za sasa za COVID-19 tulizo nazo Marekani zinafanya kazi vizuri sana katika kuzuia ugonjwa mkali, kulazwa hospitalini, na vifo, hata dhidi ya vibadala. Hata hivyo, wataalamu wa afya ya umma wanaona kupungua kwa ulinzi dhidi ya magonjwa kiasi na ya wastani ya COVID-19, haswa miongoni mwa watu walio katika hatari za juu.

Je, nibebe kitu gani wakati ninapohudhuria miadi ya dozi za kuongeza nguvu?

Tafadhali beba kitambulisho chako cha chanjo au cha mtoto wako unapoenda kuhudhuria miadi ya dozi za kuongezanguvu ilimtoahudumu uawezekuthibitishakwanza kuwa matoleo ya chanjo ya mwanzo yamekamilika. Ikiwa kitambulisho kimepotea, mtoa huduma anaweza kupitia rekodi yako.

Je, kuna tofauti gani kati ya dozi ya nyongeza na dozi za kuongeza nguvu?

Dozi ya nyongeza ni kwa ajili ya wagonjwa wenye shida ya kinga ya mwili ambao walikamilisha dozi 2 za matoleo ya chanjo ya mRNA (Pfizer au Moderna) lakini hawakuwa na mkabiliano imara wa kinga.

Dozi za kuongeza nguvu hutolewa ili kuongeza au kuimarisha ulinzi na/au kinga baada ya kupitamba kutoka upatiwe matoleo ya chanjo ya mwanzo.

Je, chapa ya chanjo ni muhimu kwenye chaguo la kuchagua dozi za kuongeza nguvu?

Unaweza kupokea dozi za kuongeza nguvu ambayo ni tofauti na matoleo ya chanjo ya msingi uliyopokea ikiwa una miaka 18 au zaidi na ukapokea Johnson & Johnson au chanjo ya mRNA ya dozi mbili wakati wa misururu yako ya msingi. Centers for Disease control and prevention (CDC, Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa) ilitoa uamuzi wao baada ya ukaguzi wenye umakini wa data ya hivi karibuni zaidi (Moderna, Johnson & Johnson, chanjo za ziada za kuchanganya na kulinganisha), na majadiliano ya kina kuhusu dozi za ziada. Novavax kwa sasa haina dozi ya ziada iliyopendekezwa na haifai kuchanganywa au kulinganishwa na chanjo nyingine za COVID-19. **Watu wenye umri wa miaka 17 au chini yake wanaweza tu kupokea chanjo ya Pfizer kwa ajili ya dozi za kuongeza nguvu ikiwa walipokea matoleo ya msingi ya Pfizer.**

Je, ni wakati gani ambapo mtu hutambulika kwamba amepata chanjo kamili?

Wewe au mtoto wako atakuwa amepata **chanjo kamili** wiki mbili baada ya kupokea dozi zote zilizopendekezwa kwenye matoleo ya chanzo za msingi za COVID-19.

Wewe au moto wako atakuwa **akienda na wakati** na chanjo ya COVID-19 pale atakapokuwa amepokea dozi zote zilizo kwenye matoleo ya msingi na [mapendekezo yote ya kuongeza nguvu](#) (Kiingereza pekee).

Je, dozi za kuongeza nguvu inaweza pokelewa sambamba na chanjo nyingine, kama vile chanjo ya mafua?

Ndiyo. Wewe au mtoto wako anaweza kupokea chanjo ya COVID-19 sambamba na chanjo nyingine. Huhitaji kupanga ratiba tofauti kati ya [chanjo zinazotakiwa shuleni \(Kiingereza pekee\)](#) za mtoto wako au chanjo nyingine zilizopendekezwa na chanjo ya COVID-19. Miadi ya chanjo ya COVID-19 ni fursa nyingine ya kujipatia au kumpa mwanao chanjo zote zinazopendekezwa.

Maswali zaidi? Tembelea:
doh.wa.gov/covidbooster